

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA TATU

04 JUNI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA TATU – TAREHE 04 JUNI, 2026

I. DUA:

II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

III. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

508. MHESHIMIWA SALEHE MBWANA MHANDO
(KILINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za Awamu ya Pili kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya vya Vuju, Mswaki na Negero katika Jimbo la Kilindi.

509. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (VWAWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha lami kutoka Vwawa - Londoni - Msia hadi Isalalo.

510. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatatua changamoto ya upungufu wa Vyumba vya Madarasa Shule ya Matala na Lositete Karatu.

511. MHESHIMIWA TWAHA SAID MWAKIOJA (MKINGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakarabati madarasa chakavu na kujenga madarasa mapya katika Shule za Msingi Jimbo la Mkinga.

OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

512. MHESHIMIWA THOMAS MGONTO KITIMA (IKUNGI MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, lini Serikali itaanza utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

WIZARA YA UCHUKUZI:

513. MHESHIMIWA MGORE MIRAJI KIGERA (MUSOMA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali imefikia wapi kuhusu Mwekezaji aliyeonesha nia ya kuwekeza Hoteli ya New Musoma ambayo ni alama ya Mji na Mkoa wa Mara.

WIZARA YA KILIMO:

514. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itajenga Bwawa la Mayuyu na Skimu ya Umwagiliaji - Korogwe Vijijini.

WIZARA YA FEDHA:

515. MHESHIMIWA KAFITI WILLIAM KAFITI (ILEMELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, lini Serikali itakamilisha Kanuni za Bima za Kilimo ili kuongeza na kupatikana kwa kinga kwa Wakulima na mazao mbalimbali.

WIZARA YA UJENZI:

516. MHESHIMIWA MOSES CHARLES BUJAGA (SUMVE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Malya – Nyambiti km 58 ili kuboresha usafirishaji katika Jimbo la Sumve.

517. MHESHIMIWA SALUM KHAMIS SALUM (MEATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza utekelezaji wa Mradi wa Barabara ya Nkoma – Lalago Km 68.

**DODOMA
04 JUNI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**